



JUMUIYA YA KIKRISTO TANZANIA

KILELE CHA MAADHIMISHO YA CCT DAY KWA MWAKA 2024

Siku ya CCT husheherekewa kila mwezi wa tano na kilele chake huwa ni Jumapili ya mwisho ya Mwezi Mei kila mwaka. Kwa mwaka 2024 Kilele cha Maadhimisho ya CCT Day imepangwa kuwa Jumapili tarehe 26 Mei kwa kila Mkoa ambapo kitaifa itafanyikia Mkoa wa Mtwara.

Lengo la maadhimisho ya Siku ya CCT (CCT Day) ni kudumisha Umoja wa CCT na kuitegemeza CCT katika utoaji wa huduma za kitume na kijamii.

Kichwa cha Neno la Mungu kitakachotumika kwenye maadhimisho ya Siku ya CCT kwa mwaka 2024 ni “Zaburi 133:1-3 “Tazama jinsi ilivyo vyema, na kupendeza, Ndugu wakae pamoja, kwa umoja.....”

CCT inatoa wito kwa kila muumini kushiriki kikamilifu katika sikukuu hii kwa kutoa sadaka maalumu kuanzia shilingi 1,000 ili kufikia malengo tuliyojiwekea.

Unaweza kuchanga kupitia Ofisi za CCT Mikoa au CCT Makao Makuu kupitia Mpesa 0743784347 JINA: JUMUIYA YA KIKRISTO TANZANIA